TANGAZO LA SERIKALI NA 100 la tarehe 17/03/2017

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 153(1)*

SHERIA NDOGO YA (UANZISHAJI WA MFUKO WA AFYA YA JAMII) ZA HALMASHAURI YA WILAYA ZA NSIMBO ZA MWAKA 2017

Jina na Tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Uanzishaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii) za Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo za Mwaka 2017, na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo-

*"Ada ya mtumiaji"* maana yake ni ada anayolipa mtumiaji wa huduma kwa Hospitali, Kituo cha afya au Zahanati, kwa ajili ya Huduma ya Afya iliyotolewa kwa mtumiaji;

Sura ya 287

"*Bodi*" maana yake ni chombo kinachosimamia Huduma za Afya ya Halmashauri iliyoundwa kwa mujibu wa kifungu Na. 88 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura Na. 287;

"*Halmashauri*" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo ;

*"Huduma za Afya"* maana yake ni huduma zote za Afya zinazotolewa na Hospitali, Vituo cha Afya, Zahanati na Kliniki maalum zinazomilikiwa na Serikali, Mashirika ya Dini, Mashirika yasiyo ya Serikali au Watu binafsi;

"*Kadi*" maana yake ni kadi itakayotolewa kwa Mwanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii;

"Kaya" maana yake ni:-

(a) Baba, Mama na Watoto wenye umri chini ya

miaka kumi na nane; na

(b) Mwanachama yeyote aliyefikia umri wa miaka kumi na nane au zaidi na awe na Mtoto au bila Mtoto mwenye umri chini ya miaka kumi na nane; au

(c) Taasisi yoyote;

"*Kituo cha Huduma kilichoteuliwa*" maana yake ni kituo kinachotoa Huduma za Afya na ni pamoja na kituo chochote kilichoanzishwa au kinachoendeshwa kwa malengo ya kutoa Huduma za Afya kinachomilikiwa na Halmashauri, Serikali, Asasi za Kidini, Mtu au Watu binafsi ambacho kinahusika na Mfuko wa Afya ya Jamii;

"*Malipo ya huduma*" maana yake ni malipo ya papo kwa papo yanayolipwa katika Kituo cha kutolea Huduma za Afya na Mtu au Watu ambao si Wanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii;

"*Mchango*" maana yake ni mchango wa fedha wa hiari, utakaotolewa na Wanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii;

"*Mganga Mkuu wa Wilaya*" maana yake ni Daktari ambaye ni Msimamizi Mkuu wa shughuli zote za Huduma za Afya katika Wilaya;

"*Mwanachama*" ni Mtu yeyote ambaye anachangia mfuko wa Afya ya Jamii;

"*Mkurugenzi*" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo au Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Taasisi" maana yake ni pamoja na Shule au Chuo kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria au Taasisi yoyote itakayokuwa imekubaliwa na kuidhinishwa na bodi kuwa Mwanachama.

"*Wizara*" maana yake ni Wizara yenye dhamana ya masuala ya Afya.

Mfuko wa Afya ya Jamii

4. (1) Kutakuwa na mfuko wa Afya ya Jamii ambao ni mpango wa hiari wenye lengo la kutoa msaada kifedha katika kugharamia matibabu, ambapo kaya zitakuwa zikilipia

Huduma za Afya, na Serikali itatoa mchango wake wa fedha kama jazilio kwa mchango kutoka kwenye Kaya Mwanachama;

(2) Matumizi ya fedha yatafanywa na kusimamiwa na Bodi kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Madhumuni ya Mfuko

5. Madhumuni ya Mfuko yatakuwa ni-

(a) Kuboresha huduma za afya katika Jamii kwa kugawanya madaraka na kuzipa nguvu Jamii katika kufanya maamuzi na kuchangia katika masuala yanayohusu afya zao;

(b) Kutoa huduma bora za afya zinazopatikana na kwa kutumia mipango endelevu; na

(c) Kutafuta vyanzo vya mapato kutoka katika Jamii kwa ajili ya kutoa huduma bora za afya kwa Wanachama;

Usimamizi wa Mfuko wa Afya ya Jamii.

6. (1) Usimamizi na uendeshaji wa Mfuko utakuwa chini ya:-

(a) Halmashauri ya Wilaya kupitia Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri ya Wilaya; na

(b) Kamati ya Maendeleo ya Kata kupitia Kamati ya Afya ya Kata, katika ngazi ya Kata;

(2) Mfuko kwa ujumla utakuwa chini ya usimamizi wa Bodi ambayo itakuwa na majukumu ya:-

(a) kuratibu shughuli zinazohusu mfuko;

(b) kusimamia, kudhibiti na kuelekeza usimamizi katika vyanzo vya mfuko;

(c) kuhakikisha kuwa mfuko unatumika na kusimamiwa kikamilifu na kwa ufanisi; na

(d) Serikali ya kijiji kupitia Kamati za Huduma za Jamii katika ngazi ya kijiji.

(2) Majukumu ya Mratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii yatakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Kufuatilia, kusimamia na kuratibu uendeshaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii kwenye vituo vya kutolea Huduma za Afya.

(b) Kuwa kiungo kati ya Halmashauri, Jamii na Wadau mbalimbali kwa ushirikiano na Mhasibu wa Mfuko, na

(c) Kuandaa taarifa za Mfuko wa Afya ya Jamii za robo na za Mwaka pamoja na majukumu mengine atakayopangiwa na Mkurugenzi.

(d) Kuhudhuria vikao vyote vya Bodi na kutoa taarifa za utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Afya ya Jamii.

Bodi

7. Kutakuwa na Bodi ya Mfuko wa Afya ya Jamii itakayoundwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi ambayo itakuwa ni chombo kinachosimamia huduma za afya katika Halmashauri.

Muundo wa Bodi

8. (1) Bodi itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Wawakilishi wanne wa Watumiaji wa Huduma za Afya, kati yao wawili lazima wawe ni Wanawake;

(b) Mwakilishi mmoja kutoka kwa Watoa huduma za afya binafsi bila faida;

(c) Mwakilishi mmoja kutoka kwa Watoa Huduma za Afya binafsi waliochaguliwa na Halmashauri kutoka katika Vituo ambavyo vina mkataba na Bodi wa kutoa Huduma za Afya ;

(d) Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Afya, Elimu na Maji;

(e) Wajumbe Wataalamu ambao ni-

(i) Afisa Mipango wa Halmashauri.

(ii) Mganga Mkuu wa Halmashauri ambaye atakuwa Katibu wa Bodi.

(iii) Mwakilishi mmoja kutoka Hospitali ya Halmashauri.

(iv) Mwakilishi mmoja kutoka Timu ya uendeshaji wa Huduma za Afya ya Mkoa.

(2) Wajumbe wa Bodi waliotajwa katika kifungu cha **8(1) (e) (i) – (v)** hawataruhusiwa kupiga kura.

(3) Mwenyekiti wa Bodi atachaguliwa kutoka miongoni mwa Wajumbe waliotajwa katika kifungu (1) (a) – (c) hapo juu.

Sifa za Wajumbe wa Bodi

9. Mjumbe wa Bodi atakuwa na sifa zifuatazo:-

(a) Awe raia wa Tanzania, isipokuwa kwa Wajumbe kutoka Mashirika yasiyo ya Kiserikali;

(b) Awe na umri usiopungua miaka ishirini na tano (25);

(c) Awe amehitimu Elimu ya Sekondari na kuendelea;
(d) Awe na uzoefu na amewahi kuonyesha uwezo wake wa kuongoza katika shughuli za huduma ya jamii;
(e) Awe na akili timamu;
(f) Asiwe amewahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai;
(g) Asiwe na wadhifa wowote katika chama chochote cha siasa.
(h) Awe Mwanachama hai wa Mfuko wa Afya ya Jamii , na
(i) Mjumbe wa kuchaguliwa awe ni mkazi wa Halmashauri.

Kazi za Bodi

10. (1) Bodi itakuwa na kazi zifuatazo:-
(a) Itasimamia masuala na shughuli zote zinazohusu Mfuko wa Afya ya Jamii ;
(b) Kusimamia Huduma za Afya katika Halmashauri;
(c) Kushauriana na Timu ya uendeshaji ya Huduma za Afya ya Halmashauri na kuhakikisha kuwa Huduma za Afya zinazotolewa ni bora na za Kitaalamu;
(d) Kukusanya na kusimamia mapato ya Mfuko wa Afya ya Jamii ;
(e) kupendekeza kwa Halmashauri Watu wanaostahili kusamehewa kutoa mchango kwenye Mfuko;
(f) kubuni malengo ya Mfuko;
(g) kupitia taarifa kutoka Kamati ya Afya ya Kata au chanzo kingine chochote;
(h) kuratibu ukusanyaji wa michango na kudhibiti matumizi; na
(i) Kupanga mipango ya afya ya Mwaka kwa ajili ya kuthibitishwa na Halmashauri;

(2) Bodi katika kutekeleza majukumu yake, itapokea na kutekeleza maagizo ya Halmashauri kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, na Taratibu.

Muda wa kukaa Madarakani

11. (1) Mjumbe wa Bodi atakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe ya uzinduzi wa Bodi na anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu (3) tu;

(2) Endapo nafasi yoyote ya Mjumbe wa Bodi itaachwa wazi kwa sababu ya kifo, kujiuzulu au kwa sababu nyingine yoyote ile, Mjumbe mwingine atachaguliwa kujaza nafasi hiyo iliyoachwa wazi kwa kipindi kilichobaki.

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2) hapo juu, haitaruhusiwa kuchagua mjumbe mwingine iwapo kipindi kilichobaki ni chini ya miezi sita.

Akaunti ya Mfuko

12. (1) Kutakuwapo na Akaunti Maalum itakayotumika na Halmashauri ambayo fedha zote zitakazokusanywa kwa ajili ya Mfuko zitahifadhiwa na kutolewa.

(2) Wawekaji saini wa Akaunti ya Mfuko watachaguliwa na Bodi na watakuwa ni wa kutoka **Kundi "A"** na **Kundi "B",** kama ifuatavyo:-

| **Kundi A** | **Kundi B** |
|---|---|
| 1. Mwenyekiti wa Bodi<br>2. Mjumbe Mmoja wa Bodi | 1. Katibu wa Bodi<br>2. Mweka Hazina wa Halmashauri |

(3) Fedha hazitatolewa kwenye akaunti ya mfuko bila saini ya mmojawapo kutoka kila Kundi.

(4) Akaunti ya Mfuko itakaguliwa kwa mujibu wa Kanuni za Fedha za Serikali.

(5)

Taarifa ya Fedha

13. Bodi itaandaa na kuwasilisha kwa Halmashauri, taarifa ya mapato na matumizi ya fedha ya kila baada ya miezi mitatu (3).

Matumizi ya Fedha za Mfuko

14. Fedha zitakazokusanywa na mfuko zitatumika kwa madhumuni yafuatayo-

(a) Masuala yanayohusiana na afya yaliyotajwa katika mpango kabambe wa afya wa Halmashauri na kuidhinishwa na Halmashauri; na

(b) Suala au shughuli yoyote muhimu ya afya itakayoonekana inafaa na kama itaidhinishwa na Bodi.

Vyanzo vya mapato

15. Vyanzo vya mapato ya mfuko vitatokana na-

(a) Fedha zote zitakazopokelewa kutokana na michango ya

Wanachama;

(b) Ruzuku kutoka Halmashauri, na Serikali Kuu, Wahisani mbalimbali toka ndani na nje ya Halmashauri;

(c) Michango ya watu binafsi wanaoishi ndani na nje ya Halmashauri;

(d) Ushuru utakaotozwa na Halmashauri kutoka vyanzo mbalimbali na kutengwa kwa ajili ya mfuko;

(e) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; na

(f) Fedha zozote halali ambazo Mfuko unaweza kupata toka mahali pengine popote.

Mipango

16. (1) Bodi itaandaa mipango ya Bajeti ya Mwaka kwa kuzingatia ratiba za vikao vya Bajeti vya Halmashauri;

(2) Bodi itapokea, itajadili, itachambua na kuidhinisha mpango wa afya na kuwasilisha kwa Halmshauri kwa ajili ya kuidhinishwa kwa kupitia Kamati za Halmashauri;

(3) Bodi itatoa maoni ya bajeti ya nyongeza kama kutakuwa na haja ya kufanya hivyo na kama mazingira yataruhusu;

(4) Mipango ya bajeti ya Mfuko itaandaliwa kulingana na utaratibu kama ulivyoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) hapo juu, ambayo ni lazima iwasilishwe Halmashauri kwa ajili ya kuidhinishwa.

Kamati ya Afya na Kata (SURA 409)

17. Kutakuwa na kamati ya Afya ya Kata kama ilivyotajwa kwenye Sheria ya Mfuko wa Afya ya Jamii.

Wajumbe wa kamati ya Afya ya Kata (SURA 409)

18. (1) Kamati ya Afya ya Kata itakuwa na Wajumbe wafuatao:-

(a) Diwani anayewakilisha Kata husika;

(b) Afisa Mtendaji wa Kata;

(c) Mwalimu Mkuu mmoja kutoka kwenye Shule ya msingi ambayo ipo kwenye Kata husika;

(d) Wajumbe wawili watakaowakilisha jamii husika ambapo mmoja wao ni lazima awe Mwanamke;

(e) Tabibu Mfawidhi au Tabibu Mfawidhi Msaidizi; wa kituo cha Afya au Zahanati, ambaye atakuwa katibu wa Kamati;

(f) Mjumbe mmoja atakayeteuliwa na kamati ya maendeleo ya kata kutokana na watu waliopendekezwa na Kamati za Kata zilichomo ndani ya eneo la Kata; na

(g) Mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Kamati ya maendeleo ya Kata kutoka kwenye vyama vya kijamii kutoka kwenye Kata.

(2) Mwenyekiti wa Kamati ya Afya ya Kata atachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe lakini asiwe Diwani, Mtendaji wa Kata au Mtendaji wa Mtaa;

(3) Endapo Kamati ya Afya ya Kata itashindwa kutekeleza kazi zake, Bodi itatoa onyo au kuivunja na Halmashauri itafanya utaratibu wa uchaguzi wa wajumbe wengine katika muda usiozidi miezi mitatu (3) tangu tarehe ya kuvunjwa kwa Kamati hiyo.

Kazi na majukumu ya Kamati ya Afya ya Kata.

19. (1) Kamati ya Afya ya Kata itakuwa na majukumu yafuatayo:-

(a) Kuhamasisha na kuandaa Jamii kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii ;

(b) Kuandaa na kuthibitisha orodha na kuratibu idadi ya Wanachama wa Mfuko wa Afya wa Jamii ;

(c) Kusimamia ukusanyaji wa michango ya Mfuko;

(d) Kuratibu viwango vya uchangiaji kwenye Huduma za Afya;

(e) Kupitia utendaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii na kutoa mapendekezo na ufumbuzi kwa Halmashauri kupitia Bodi ya Afya;

(f) Kuanzisha na kuratibu Mipango ya Afya na Jamii na,

(g) Kuendesha mikutano ya Wanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii ndani ya Kata.

(2) Kamati ya Afya ya Kata, itakaa kila baada ya miezi mitatu (3) na Katibu atatoa taarifa ya maandishi siku saba (7) kabla ya siku ya kikao.

Utoaji wa Huduma za Afya.

20. Kila Mwanachama-

(a) Atakuwa na haki ya kisheria kupata Huduma ya Afya aliyolipia kabla ya kuugua ndani ya eneo la Halmashauri

au eneo lingine lolote kadri itakavyo kubaliwa,

(b) Atakuwa na haki ya kutoa mapendekezo kuhusu Huduma za Afya kupitia kamati husika ambayo yatafanyiwa kazi na Bodi; na

(c) Atashirikishwa kikamilifu katika uandaaji na utekelezaji wa mpango wa upatikanaji wa Huduma za Afya katika eneo la Halmashauri.

Mchango wa Mwanachama

21. (a) Mtu yeyote atakayetaka kuwa Mwanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii atapaswa kulipa kila mwaka mchango kiasi cha Shilingi elfu kumi na tano tu (15,000/=)

(b) Viwango hivi vinaweza kufanyiwa marekebisho na Halmashauri wakati wowote iwapo itaonekana kuna umuhimu wa kufanya marekebisho hayo.

Muda wa Uanachama

22. (a) Mtu yeyote atabaki kuwa Mwanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii kila atakapo lipa mchango wake wa Uanachama, na

(b) Kila Mwaka utakapoisha Uanachama wa mtu utafikia mwisho hadi pale atakapotimiza masharti ya kifungu (a) hapo juu.

Malipo ya Papo kwa papo

23. (1) Mtu yeyote ambaye hatakuwa Mwanachama wa mfuko huu atalipa malipo ya papo kwa papo kila atakapoenda kupata matibabu katika kituo cha kutolea Huduma za Afya.

(2) Malipo ya papo kwa papo yatalipwa kwa ajili ya kusajiliwa, kumwona Daktari, na kupewa dawa kwa mujibu wa viwango vitafuatavyo;-

(a) Hospitali shilingi elfu nane (8,000/=);
(b) Vituo ya Afya shilingi elfu tano ( 5,000/=);
(c) Zahanati elfu tatu (3,000/=).

Utaratibu wa Misamaha

24. Misamaha kwa wasioweza kulipia gharama za matibabu utatolewa na kulipiwa na Halmashauri baada ya kuzingatia utaratibu ufuatao:-

(a) Serikali ya Mtaa katika vikao vyake itawatambua, kuwajadili na kuwasilisha mapendekezo ya Orodha ya majina ya watu wanaostahili kupewa Msamaha kwenye

Kamati ya Maendeleo ya Kata,

(b) Kamati ya Maendeleo ya Kata itawajadili wale wasioweza kulipia gharama na kuthibitisha orodha yao na kuiwasilisha kwenye Bodi, na

(c) Bodi ya Afya itapokea na kujadili mapendekezo husika na kuyawasilisha pamoja na gharama zake kwa Halmashauri kwa ajili ya kulipiwa.

Utoaji wa Kadi kwa Mwanachama

25. (1) Kila Kaya Mwanachama wa Mfuko atapewa kadi baada ya kulipa mchango wake wa Mwaka wa Shilingi elfu kumi na tano (15,000/=) au kiwango kitakachopendekezwa na Bodi na kuidhinishwa na Halmashauri.

(2) Kila mtu atakayesamehewa kulipa mchango atapewa kadi ya Uanachama na Halmashauri italipa gharama ya kadi hiyo.

(3) Viwango vya kulipia uanachama vitapendekezwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata na kujadiliwa na Bodi kisha kuidhinishwa na Halmashauri.

Makosa na Adhabu

26. Mtu yeyote ambaye:-

(a) atakwenda kinyume na masharti yoyote ya Sheria Ndogo hizi;

(b) atafanya kitendo chochote ambacho kitazuia Bodi kufanya kazi zake kwa ufanisi;

(c) atatumia vibaya mali na rasilimali za Mfuko;

(d) atafanya udanganyifu ili aweze kunufaika na Huduma za Afya zitolewazo kwa utaratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii; au

(e) atazuia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

Atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu **(**300**,**000**/=),** au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili (12) au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe .................. na kubandikwa mbele ya:-

MWAILWA SMITH PANGANI,
*Mkurugenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo*

RAPHAEL A. KALINGA,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo*

NAKUBALI,

Dodoma,
9 Januari, 2017

GEORGE B. SIMBACHAWENE,
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tamisemi*